# Simoni Mkirene

Mtazamo Wa Ibada Katika

Mtu Aliyebeba Msalaba wa Yesu

**F. Wayne Mac Leod**

**LIGHT TO MY PATH BOOK DISTRIBUTION**

Sydney Mines, Nova Scotia, CANADA B1V 1Y5

Simoni Mkirene

Hakimiliki © F. Wayne Mac Leod

Toleo la smashwords, maelezo ya leseni.

Kitabu hiki kime ruhusiwa kwaajili ya starehe yako binafsi. Kitabu hiki hakiuzwi tena wala kugawiwa kwa mtu mwingine. Kama utapenda kugawa kwa watu wengine tafadhari nunua vingine kwaajili ya kila mmoja. Kama unasoma kitabu hiki na hujakinunua au hakikununuliwa kwaajili ya kukitumia wewe. Tafadhari rudi kwenye duka lako la vitabu na ununue chako. Asante kwa kuheshimu kazi nzuri ya mwandishi.

Haki zote zimehifadhiwa. Hakuna sehemu ya kitabu hiki inaweza kunakiliwa au kusambazwa kwa namna yoyote au njia yoyote ile bila idhini ya maandishi ya mwandishi.

Biblia takatifu,toleo la kingereza® (ESV®) hakimiliki© ya crossway, huduma ya usambazaji wa habari njema. Haki zote zimehifadhiwa. ESV ujumbe toleo 2007

# Yaliyomo

Dibaji....................................................................................5

Sura ya 1 – Kuna Nini Katika Jina? ........................................................7

Sura ya 2 – Kushurutishwa Kumfuata Yesu..........................................13

Sura ya 3 - Kubeba Msalaba ..................................................................19

Sura ya 4 - Amesikia...............................................................................25

Sura ya 5 - Kukabidhi Msalaba..............................................................29

Light To My Path Book Distribution .....................................................35

# Dibaji

Simoni Mkirene ni mhusika asiyejulikana wa Biblia ambaye alikuwa na jukumu kubwa la kutekeleza wakati wa kusulubiwa kwa Yesu. Injili tatu kati ya nne zinataja jina lake na ukweli kwamba alibeba msalaba wa Yesu, lakini kuna mambo machache sana yanayojulikana kuhusu yeye.

Imefichwa katika mistari michache ya Maandiko yanayotaja jina lake kuna mambo fulani yakupendeza kuhusu kazi ambayo Yesu alitekeleza siku hiyo. Jukumu la Simoni halikuwa tu kumhudumia Bwana Yesu kwa kubeba msalaba wake bali pia kutuonyesha jambo fulani kuhusu kazi ambayo Kristo alitimiza kwa niaba yetu.

Lengo la somo hili fupi juu ya mtu wa Simoni Mkirene ni kuona umuhimu wake katika kumfunua Kristo na huduma yake. Bwana na kubariki kazi hii kwa utukufu wa jina lake. Mungu akubariki,

F. Wayne Mac Leod

# Sura ya 1 – Kuna Nini Katika Jina?

Tunasoma kuhusu Simoni MKirene katika Injili tatu kati ya nne.

*[32] Hata walipokuwa wakitoka, wakamwona mtu Mkirene, jina lake Simoni; huyu wakamshurutisha auchukue msalaba wake. (Mathayo 27)*

*[21]Wakamshurutisha mtu aliyekuwa akipita, akitoka mashamba, Simoni Mkirene, baba yao Iskanda na Rufo, ili auchukue msalaba wake. (Marko 15)*

*[26]Na walipokuwa wakimwondoa walimkamata mtu mmoja, Simoni Mkirene, aliyekuwa ametoka shamba, wakamtwika msalaba, auchukue nyuma yake Yesu. (Luka 23).*

Kila kitu tunachojua kuhusu mhusika huyu asiyejulikana kinapatikana katika aya hizi tatu. Kazi yetu ni kuchunguza kile ambacho mistari hii inatuambia ili kuona kile tunachoweza kugundua kuhusu Simoni na jukumu alilofanya wakati wa kusulubishwa kwa Yesu. Tuanze na jina lake.

*Simon*

Inaaminika kwa ujumla kwamba jina Simoni ni la asili ya Kiebrania. Limetokana na jina Shim'on linalomaanisha "amesikia." Rejeo la kwanza la jina Simoni linapatikana katika Mwanzo 29:33. Alikuwa mwana wa Ibrahimu kupitia kwa mkewe, Lea:

*[33]Akapata mimba tena akazaa mwana, akasema, Kwa kuwa*

*Bwana amesikia ya kwamba mimi sikupendwa, amenipa na huyu; akamwita jina lake Simeoni. (Mwanzo 29)*

Lea akamwita mtoto wake Simeoni kwa sababu Mungu alisikia maombi yake kwa ajili ya mtoto na alijua kwamba hapendwi.

Kulingana na Wikipedia, lilikuwa mojawapo ya majina maarufu ya Kiyahudi katika karne ya kwanza miongoni mwa Wayahudi wa Kipalestina (https://en.wikipedia.org/wiki/Simon_(given_name).

Hii inatuambia nini kuhusu Simoni mkirene ni kwamba alikuwa na jina la Kiebrania. Katika siku zetu, tunatumia majina kutoka asili tofauti. Hii haikuwa hivyo sana katika siku ambazo Simon aliishi. Katika siku hizo, ilikuwa rahisi kuamua uraia wamtu kwa jina aliloitwa. Inaonekana kwamba wakati huo Simoni alikuwa wa ukoo wa Kiyahudi.

*MKirene*

Simoni hatajwi kamwe katika Maandiko kwa jina lake la kwanza pekee. Daima anaitwa Simoni Mkirene au Simoni kutoka eneo la Kirene.

Kirene ilikuwa kwenye pwani ya Kaskazini ya Afrika katika nchi ya sasa ya Libya. Ilianzishwa na Wagiriki katika Karne ya 7 KK na ilikuwa na umuhimu fulani wa kilimo wakati huo. Hatimaye ilikuwa sehemu ya Milki ya Kirumi. Kufikia wakati wa Agano Jipya, mji wa Kirene ulikuwa na idadi kubwa ya Wayahudi. (Philip W. Comfort, Ph.D., Walter A. Elwell, Ph.D. (ed), “Cyrene,” Tyndale Bible Dictionary,

Electronic Edition, L A R I D I A N: Cedar Rapids, Iowa, 2001).

Inawezekana kwamba baadhi ya Wayahudi hao kutoka Kirene walikuja Yerusalemu kusherehekea Pasaka katika siku ambazo Yesu alisulubiwa.

Ingawa jina lake linaonyesha kwamba Simoni alitoka Kirene, haiko wazi katika Maandiko kuwa alitoka tu kuja Yerusalemu kwa ajili ya Pasaka au alikuwa amehama kutoka Kirene na kuishi katika eneo hilo. Marko anatuambia kwamba Simoni Mkirene alikuwa baba wa Aleksanda na Rufo.

*[21] Wakamshurutisha mtu aliyekuwa akipita, akitoka mashamba, Simoni Mkirene, baba yao Iskanda na Rufo, ili auchukue msalaba wake. (Marko 15)*

Marko 15 inaeleza Simoni kama "mpita njia" ambaye alikuwa anatoka Kirene. Jinsi Marko anavyosema kuhusu Simoni inaonekana inaonyesha kwamba hakuwa mtu anayejulikana sana wakati huo. Alikuwa mpita njia kwa wengi waliomwona siku hiyo. Pia alikuwa mgeni ambaye hakuwa amekulia Yerusalemu.

Ingawa Marko anapata ugumu kueleza Simoni alikuwa nani, hivi sivyo ilivyo kwa wanawe. Wanatajwa kwa majina yao ya kwanza, Alexander na Rufo. Marko anamtambulisha Simoni kupitia wanawe, ambao wanaonekana kujulikana zaidi.

Tunalo rejeo katika Matendo 19:33 kwa kiongozi wa Kiyahudi kwa jina Alexander, ambaye aliitwa kuwatetea Wayahudi katika wakati wa ghasia huko Efeso. Paulo alituma salamu kwa mtu mmoja jina lake Rufo na mama yake katika Warumi 16:13. Ingawa ni vigumu

kusemaikiwa watu hawa walikuwa wana wa Simoni Mkirene, kifungu hicho kinaonekana kudokeza angalau kwamba wana wa Simoni walijulikana katika jumuiya wakati huo.

Ukweli wa kwamba watu walionekana kuwajua wana wa Simoni unatufanya tujiulize jinsi hali hii ingeweza kuwa kesi ikiwa hawakuishi katika eneo la Yerusalemu. Je, inawezekana kwamba Simoni alihamia eneo hilopamoja na familia yake kutoka Kirene? Hatuna jibu la wazi kwa swali hili.

Tunachojifunza kuhusu Simoni katika mistari hii ni kwamba inaelekea alikuwa Myahudi aliyeishi Kirene huko Afrika Kaskazini. Alikuwa na wana wawili wanaoonekana kujulikana huko Yerusalemu. Ingawa hatujui kama aliishi kwa kudumu katika eneo hilo au kutembelea tu, alikuwepo wakati wa kusulubiwa kwa Kristo. Ilikuwa ni mtu huyu asiyejulikana ambaye alichaguliwa na Mungu kubeba msalaba wa Bwana Yesu njiani kuelekea Kalvari.

Yakuzingatia:

Jina la Simoni linatufundisha nini kuhusu yeye na chimbuko lake?

Fikiria ukweli kwamba Myahudi kutoka Libya ya sasa alichaguliwa kubeba msalaba wa Yesu. Hatuna dalili ya Simoni kumjua Yesu. Je, hii inatuambia nini kuhusu aina ya watu ambao Mungu huchagua kwa kusudi Lake?

Maombi:

Mshukuru Bwana kwa kuwa huwafikia watu wasiowezekana na kuwatumia kwa kusudi lake. Mshukuru kwa jinsi alivyokuchagua wewe kuwa mtoto wake. Mwambie akupe maana ya kusudi lake kwa maisha yako.

Mungu huwatumia watu kwa njia tofauti. Alimchagua Simoni kubeba mzigo mzito kwa ajili ya Bwana Yesu. Je, uko tayari kubeba wajibu ambao Mungu amekupa? Je, utachukua msalaba wako kumfuata kama Simoni alivyofanya?

# Sura ya 2 – Kushurutishwa Kumfuata Yesu

Injili mbili zinatuambia kwamba, wakati wa kusulubishwa kwa Yesu, Simoni alikuwa "akija kutoka mashambani" (Marko 15:21; Luka 23). Neno la Kigiriki linalotumiwa kumaanisha "nchi" katika mistari hii ni neno "agros" linalorejelea shamba au kipande cha ardhi inayolimwa.

Biblia haituambii kwa nini Simoni alikuwa mashambani. Je, aliishi huko? Alikuwa anafanya kazi shambani? Je, alikuwa anarudi kutoka mashambani kwenda nyumbani mjini? Hatujui. Marko anamfafanua Simoni, hata hivyo, kuwa "mpita njia." Neno hili linaweza kutupa kumfahamu zaidi Simoni.

Fikiria yaliyokuwa yakitokia wakati Simoni alipokuwa akitoka mashambani na kuingia katika jiji la Yerusalemu. Askari wa Kirumi walikuwa wamemdhihaki na kumpiga Yesu. Sasa walikuwa wakimpeleka katika mitaa ya Yerusalemu hadi kwenye kilima cha Kalvari. Watu walisimama kando ya barabara, wakitazama msafara huu. Macho yote yalikuwa yakimtazama Yesu alipokuwa akibeba msalaba wake njiani kuelekea kuuawa.

Ni katika muktadha huu tunasoma katika Marko 15:21, "Wakamshurutisha mtu aliyekuwa akipita, akitoka mashamba, Simoni Mkirene, baba yao Iskanda na Rufo, ili auchukue msalaba wake." Simon ni mpita njia. Kwa maneno mengine, halikuwa kusudi lake kutazama

kile kilichokuwa kikiendelea. Alikuwa akielekea kwenye jambo lingine, na msafara huu ulikuwa ni msumbufu tu katika utaratibu wake. Kama mpita njia, hakuwa amekuja kumuona Bwana akienda msalabani. Huenda hakupendezwa hasa na kile kilichokuwa kikitokea siku hiyo. Alikuwa na mambo mengine ya kufanya.

Wakati Simoni alikuwa na mambo mengine akilini mwake siku hiyo, Mungu alikuwa na kusudi kwa siku yake. Katika simulizi ya Yohana ya maandamano ya kwenda Kalvari, anatuambia kwamba Yesu alibeba msalaba wake mwenyewe:

*[17]Akatoka, hali akijichukulia msalaba wake, mpaka mahali paitwapo Fuvu la Kichwa, au kwa Kiebrania, Golgotha. (Yohana 19)*

Kutoka katika Injili nyingine, tunaona kwamba askari walimkuta Simoni Mkirene na kumlazimisha kubeba msalaba wa Yesu. Hakuna utata hapa. Yesu alianza kwa kubeba msalaba wake, lakini kwa sababu alikuwa dhaifu kutokana na kipigo alichopewa na askari, hakuweza kuendelea.

Walipoona kwamba Yesu ameshindwa kubeba msalaba Wake, askari wakaenda nje kati ya umati wa watu wakimtafuta mtu ambaye angeweza kubeba kwa ajili yake. Simoni, ambaye alikuwa akipita wakati huo, ndiye mtu waliyemchagua. Maneno yaliyotumiwa kuelezea pambano kati ya Simoni na askari wa Kirumi ni muhimu. Mathayo na Marko wote wanatuambia kwamba "walimlazimisha" Simoni kubeba msalaba wa Yesu (ESV). Luka anasema kwamba "walimkamata" Simoni na kuweka msalaba juu yake.

Askari hawakuwa wanatafuta mtu wa kujitolea kubeba msalaba kwa

ajili ya Yesu. Walimlazimisha Simon kubadili mipango yake na kuuchukua msalaba ule. Wazo ni kwamba ikiwa hatasikiliza walichomwambia afanye, kungekuwa na athari. Simoni hakuchagua kubeba msalaba wa Yesu. Msalaba ulichaguliwa kwa ajili yake.

Hapa mbele yetu, tunayo picha ya mtu ambaye anaendelea na shughuli zake za kawaida. Hakuwa na hamu na Bwana Yesu na kile kilichokuwa kikitokea Kwake. Yesu alikuwa mgeni kwake. Mungu, hata hivyo, alikuwa na mpango kwa ajili ya Simoni. Wakati wa ziara yake Yerusalemu alikuwa mkamilifu. Alikuwa mahali pazuri kwa wakati huo. Uamuzi wa kutafuta mtu wa kubebea msalaba kwa ajili ya Yesu ulionekana kuwa haukupangwa. Yesu alipokuwa akihangaika na kujikwaa na msalaba, askari waliosimamia walifanya uamuzi wa haraka haraka kupata mtu wa kumbebea. Wakatoka nje na kuingia katika umati wa watu, wakamwona Simoni. Wakamkamata na kumuwekea msalaba ule mgongoni.

Hakuna lolote kati ya haya lililotokea kwa bahati mbaya. Nyuma ya tendo hili la huruma kwa Yesu kulikuwa na mkono wa Baba. Mungu alijua kabla ya Simoni kuondoka mashambani ni kitu gani ambacho kilikuwa kinamngojea. Alimchagua kubeba msalaba kwa ajili ya Mwanawe. Simon alikuwa hajui kabisa jambo hilo alipoondoka kuelekea mjini. Askari hawakujua uongozi wa Mungu walipoingia kwenye umati kutafuta mtu wa kubeba msalaba hadi Kalvari.

Simon alikuwa akiendelea na kazi yake ya kawaida. Hakuwa na hamu na Yesu. Alikuwa akipita pale utaratibu wake ulipokatizwa.Kwa mwonekano wa kibinadamu, mipango yake ilikatishwa na askari wa Kirumi, kulikuwa na kitu zaidi ya kukutana na hilo lililokuwa

likifanyika. Mungu alikuwa anamwendea Simoni.

Bwana Yesu, akizungumza katika Yohana 15, alisema:

*[16]Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa; ili kwamba lo lote mmwombalo Baba kwa jina langu awapeni. (Yohana 15)*

Akiwaandikia Wakolosai, mtume Paulo alisema:

*[2:1] Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi [2] mliziendea zamani kwa kuifuata njia ya ulimwengu huu, kwa kumfuata mkuu wa uwezo wa anga, roho yule atendaye kazi sasa ndani ya wana. wa kuasi, [3]ambao sisi sote tuliishi kati yao hapo kwanza katika tamaa zetu, tukizifuata tamaa za mwili na nia; na kwa asili tulikuwa wana wa ghadhabu, kama wanadamu wengine. [4]Lakini Mungu, kwa kuwa ni mwingi wa rehema, kwa mapenzi yake makuu aliyotupenda; [5]hata tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu, alituhuisha pamoja na Kristo; mmeokolewa kwa neema.(wakolosai 2)*

Kama vile askari hao walivyomlazimisha Simoni kuchukua msalaba na kumfuata Yesu, ndivyo Roho wa Mungu anavyoendelea kuwashurutisha wale ambao hawapendezwi na Kristo kumfuata leo. Mtume Paulo alikuwa akielekea Damasko kuwatesa wale walioifuata njia ya Kristo alipokutana na Mwokozi. Siku hiyo, Bwana alimlazimisha kujisalimisha, kuuchukua msalaba wake na kumfuata. Paulo hangekuwa vile vile tena.

Mpango wa Simoni wa siku ulibadilishwa. Alikuwa mtu

asiyependezwa ambaye alikutana na Mwokozi akiwa njiani kuingia katika jiji la Yerusalemu. Hili halikuwa jambo alilochagua mwenyewe. Ikiwa angekuwa yeye, angeendelea na safari yake bila hata kutazama mwelekeo wa Yesu. Hata hivyo, hilo halikuwa kusudi la Mungu kwake. Mungu alikutana na Simoni kwa kutojali kwake na kumfanya sehemu ya tukio moja kubwa katika historia ya mwanadamu.

Simonini picha yako na mimi. Tunapitia maisha ya shida tukimfikiria Bwana Yesu na kazi Aliyofanya. Kama vile Simoni akimpita Bwana Yesu njiani kuelekea msalabani, sisi pia tunapita bila kutambua umuhimu wa kile kilichotokea siku hiyo. Ni kana kwamba kusulubishwa hakukuwa na uhusiano wowote nasi. Isingekuwa kazi ya Mungu katika kutulazimisha kuuzingatia msalaba; tungeendelea na njia yetu bila kuelewa kwamba Mwokozi alikuwa akienda msalabani kwa ajili yetu.

Ni watu wangapi wanaotuzunguka walio kama Simoni—wasiojali Mwokozi na msalaba Aliobeba? Jinsi tunavyohitaji kumshukuru Bwana kwamba anakutana nasi katika kutojali kwetu. Simoni ni picha ya neema ya Mungu katika kuwashurutisha wasioamini kuchukua msalaba wao na kumfuata Yesu.

Yakuzingatia:

Je, tuna ushahidi gani kwamba Simoni hakupendezwa hasa na kusulubishwa kwa Bwana Yesu?

Je, Mungu anatulazimisha kuuchukua msalaba wetu na kumfuata? Ikiwa Mungu hakutulazimisha, je, tungekuwa na nafasi ya kumjua Kristo?

Je! ni kwa jinsi gani Simoni ni picha ya neema ya Mungu katika kujidhihirisha kwa wale ambao hawana hamu naye?

Maombi:

Chukua muda wa kumshukuru Bwana kwamba alitufikia wakati hatukuwa na hamu naye.

Mshukuru Bwana kwa jinsi alivyopanga matukio na hali zilizokuleta kwake.

Je, una marafiki au jamaa ambao, kama Simoni, hawapendezwi na Bwana na kazi Yake? Mwambie Bwana awafikie na kuwalazimisha kumwangalia.

# Sura ya 3- Kubeba Msalaba

Mathayo, Marko na Luka wote wanatuambia kwamba askari "walimlazimisha" Simoni kubeba msalaba wa Yesu. Ingawa haijaelezewa wazi hapa, kihistoria, kwa sababu msalaba wote ulikuwa mzito sana, mtu aliyehukumiwa angebeba tu boriti hadi mahali pa kusulubiwa.

*Katika visa vingine, waliohukumiwa walilazimishwa kubeba msalaba hadi mahali pa kunyongwa. Msalaba mzima ulikuwa na uzito wa zaidi ya kilo 135 (lb 300), lakini boriti haikuwa mzigo mzito, uzani wa karibu kilo 45 (lb 100). (https://en.wikipedia.org/wiki/Crucifixion)*

Kwa kuwa uzitowa msalaba mzima labda ulikuwa zaidi ya pauni 300. (kilo 136), nguzo pekee ndiyo iliyobebwa. Upau wa msalaba, uzito wa lb 75 hadi 125. (kilo 34 hadi 57), uliwekwa kwenye nepe ya shingo ya mwathirika na kusawazishwa kwenye mabega yote mawili. Kawaida, mikono iliyonyoshwa kisha ilifungwa kwenye upau wa msalaba. (https://www.cbcg.org/scourging-crucifixion.html)

Ingekuwa ni jambo la kufedhehesha kwa mhalifu kubeba msalaba ambao angesulubishwa barabarani hadi eneo la kifo chake. Kusudi lilikuwa kumfanya mhasiriwa ahisi kushindwa kwake na kutokuwa na msaada. Hii iliongeza tu ukatili na uchungu wa kusulubiwa.

Yohana 19:17 inatuambia kwamba Yesu alipoanza safari ya kwenda Golgotha, aliubeba msalaba. Wakati fulani katika safari hii, hata hivyo, uliwekwa kwenye mabega ya Simoni Mkirene ambaye

alichukua umbali iliyobaki.

Ilipofika wakati wa kusulubishwa kwa Bwana Yesu, hakuna chochote kilichoachwa kwa bahati. Kila kitu kilikuwa na umuhimu wake. Ninaamini ya kwamba Bwana alikuwa na kusudi la Simoni. Alikuwa chaguo la Mungu kubeba msalaba wa Yesu njia iliyobaki. Ni muhimu kuelewa kinachoendelea hapa.

Wakati askari walipomfunga Bwana Yesu msalaba, ni Simoni ambaye angeuleta Kalvari. Maelezo haya hayawezi kwenda bila kutambuliwa. Ni mtu mwenye hatia ndiye aliyebeba msalaba. Mtu mwenye hatia, hata hivyo, hakuwa Bwana Yesu - alikuwa Simoni. Simoni ndiye aliyehitaji msamaha.

Simon hakuwa mtu pekee mwenye hatia. Aliwakilisha binadamu wote. Kumbuka kwamba inaelekea Simoni alikuwa Myahudi. Pia alikuwa anatoka nchi ya kigeni ya Kirene huko Afrika. Simoni aliwawakilisha Wayahudi na wageni wa Afrika na kwingineko. Alituwakilisha mimi na wewe.

Siku hiyo Simoni alipokuwa akiubeba msalaba wa Yesu, Baba alikuwa akiuambia ulimwengu kwamba Mwanawe hakuwa mhusika mwenye hatia. Yule aliyebeba msalaba ndiye aliyehitaji kufa. Simoni alibeba msalaba huo kama mwakilishi wa Wayahudi na wageni. Umati ulipomtazama Simoni, akiwa ameelemewa na msalaba, waliona picha yao wenyewe. Katika picha hiyo, waliona mtu mwenye dhambi akibeba mzigo wa dhambi yake. Waliona hukumu ya Mungu juu ya wanadamu. Mungu alikuwa anawaonyesha kwamba wao ndio waliostahili kubeba msalaba huu na kubeba adhabu yake.

Luka anatuambia kwamba msalaba uliwekwa juu ya Simoni, na alilazimika kuubeba nyuma ya Yesu.

*[26]Na walipokuwa wakimwondoa walimkamata mtu mmoja, Simoni Mkirene, aliyekuwa ametoka shamba, wakamtwika msalaba, auchukue nyuma yake Yesu. . (Luka 23)*

Yesu alimwongoza Simoni hadi mahali pa kuuawa. Kwa kufanya hivyo, Baba alikuwa anatuonyesha kile tulichostahili. Adhabu ya dhambi ni mauti. Simoni alipokuwa akimfuata Bwana Yesu hadi Golgotha, alikuwa akijionea mwenyewe jinsi ilivyokuwa kuhukumiwa kifo. Lazima alihisi kitu fulani cha uchungu wa Yesu alipokuwa akijiandaa kujilaza juu ya msalaba huo.

Ujumbewa injili wakati mwingine umetiwa maji hadi mahali ambapo uhalisi wa dhambi na hukumu umepunguzwa. Hatupendi kuwaambia watu wao ni wenye dhambi wanaostahili ghadhabu ya Mungu. Injili tunayohubiri ni injili ya baraka na mafanikio. Tunawaambia watu waje kwa Kristo na wapate maisha mazuri. Ingawa hatuthubutu kuhoji faida za ajabu ambazo ni zetu katika Bwana Yesu, ukweli wa hatia yetu haupaswi kupuuzwa kamwe.

Mpaka tuelewe hatia yetu, hatutawahi kushika utimilifu wa neema ya Kristo. Tunasitisha tukio kwa muda kidogo mahali ambapo Simoni anaongozwa na Kristo hadi mahali pa kuuawa. Kiunzi kilicho mbele yetu ni cha Simoni aliyebeba msalaba. Anatuwakilisha sisi sote. Myahudi na mgeni wote walikuwa na hatia mbele za Mungu. Tulistahili msalaba huo. Tunasimama kwenye kilima cha Golgotha tukiwa na uzito wa mzigo huo mabegani mwetu tukielewa vyema

hukumu ya Mungu juu ya maisha yetu.

Je, tumejihusisha na kifo cha Kristo? Je, tunafahamu ukweli kwamba tulistahili msalaba huo? Je, tunaelewa aibu iliyokuwa yetu na bei tuliyopaswa kulipa? Je, tumehisi uzito wa boriti hiyo ya msalaba kwenye mabega yetu? Jinsi ilivyo rahisi kwetu kuuchukulia wokovu wetu kuwa wa kawaida. Mungu atujalie ufahamu wa kina wa dhambi zetu ili neema yake iweze kukuzwa.

Yakuzingatia:

Kwa nini unadhani Mungu aliona vyema kumwita Simoni aubebe msalaba wa Yesu? Je, yeye ni picha yangu na wewe?

Je, kuna umuhimu gani kwetu kuelewa dhambi na hatia yetu mbele za Mungu? Je, kanisa limekuwa liaminifu katika kuhubiri kuhusu dhambi?

Je, kweli tunaweza kuthamini neema ya Kristo ikiwa hatuelewi hatia yetu?

Maombi:

Mwambie Bwana akupe uthamini wa ndani zaidi wa kile alichokufanyia katika kuchukua nafasi yako msalabani.

Tumwombe Mungu atujalie sisi waumini ufahamu mkubwa zaidi wa dhambi na matokeo yake katika maisha yetu.

# Sura ya 4- Amesikia

Katika sura ya 1, tulizungumza kuhusu jina Simoni. Jina hilo ni la asili ya Kiebrania na linatokana na neno linalomaanisha “kusikia.” Neno ambalo jina limetoka limefafanuliwa kama ifuatavyo:

Wazo ni kwamba mtu anayesikiliza hufanya hivyo kwa nia ya kufanya jambo fulani kuhusu kile anachosikia. Usikilizaji huu sio tu juu ya kuelewa maneno lakini juu ya kutuliza maumivu na mateso au kujibu mahitaji yaliyofunuliwa katika maneno yaliyosemwa.

Lea alipompa mwanawe jina la Simeoni, alifanya hivyo kwa kutambua kwamba Bwana Mungu amesikia kwamba hapendwi. Katika mawazo ya Lea, Mungu alipompa mwana, Alikuwa akifanya hivyo kwa sababu Alisikia hitaji lake na alifikia kwa huruma na rehema kushughulikia maumivu yake.

Kwa nini ni muhimu kwamba tuzingatie maana na asili ya jina la Simoni katika muktadha huu? Hebu tusitishe tukio tena na tuchunguze kinachoendelea. Hapa mbele yetu ni mtu mmoja jina lake Simoni. Jina lake linamaanisha, "amesikia." Mtu huyu amebeba msalaba wa Yesu wanaposonga polepole kuelekea mahali pa kunyongwa.

Kwa mwonekano wote wa nje, hii ni picha ya kushindwa. Yesu anakaribia kufa mikononi mwa askari-jeshi la Waroma. Idadi ya watu wa Yerusalemu kwa kiasi kikubwa imekataa ujumbe aliokuja kuhubiri. Viongozi wa kidini walimgeuzia kisogo na madai yake ya kuwa Masihi. Waliwajibika kwa hukumu yake ya kifo. Walisimama sasa wakifurahia

kile walichokiona kama kushindwa Kwake.

Hata hivyo, isiyoonekana kwa Wayahudi na maofisa wa Kirumi, ilikuwa ishara yenye nguvu kutoka kwa Mungu. Yesu alipokuwa akienda msalabani, alifuatwa na mtu ambaye jina lake lilimaanisha, "amesikia." Fikiria hili kwa muda. Kilichochukuliwa na macho ya mwanadamu kuwa kushindwa kabisa kilikuwa, kwa kweli, njia ya Mungu ya kuuambia ulimwengu kwamba alikuwa amesikia kilio chao. Alielewa hitaji lao. Kama vile Simoni, ambaye aliwakilisha mataifa ya Kiyahudi na ya kigeni ya wakati huo alipomfuata Yesu hadi msalabani, Baba alikuwa akisema, "Nimeelewa hitaji lako, nami nimesikia."

Neno ambalo jina la Simoni lilitolewa lilizungumza sio tu juu ya kusikia kwa sikio lakini pia kujibu kwa huruma na rehema. Maneno, "amesikia" yanatuelekeza moja kwa moja kwa Yesu. Alikuwa jibu la Baba. Vilio vya waliopotea vilifika masikioni mwa Baba, na kwa kujibu, akamtoa Mwanawe wa pekee kuwa jibu la uchungu na upotevu wa ulimwengu.

Kwa Wayahudi, Yesu alisulubishwa kwa sababu alijitangaza kuwa Mungu. Kwa Warumi, ilikuwa ni kwa sababu alikuwa msumbufu. Kwa Baba, hata hivyo, ilikuwa ni kwa sababu alikuwa amesikia vilio vya wanadamu waliopotea katika dhambi.

Simoni alipokuwa akiubeba msalaba, alikuwa akitoa kauli kuhusu Yesu. "Amesikia kilio chetu," akasema. Huyu Yesu anayeenda mbele yangu anaelewa hitaji lako na amekuja kufanya jambo juu yake. Atakufa, si kwa sababu ya jambo lolote ambalo amefanya bali kwa sababu anataka kutoa suluhisho la kutengwa kwetu na Mungu.

Anakuja kuleta msamaha na urejesho. Anakuja kuleta utakaso na uponyaji. Anakuja kwa sababu amesikia kilio chetu cha kukata tamaa.

Sidhani kama Simoni alielewa umuhimu wa jina lake alipomfuata Bwana Yesu hadi Golgotha. Siamini umati wa watu ulizingatia pia. Mbele yao, hata hivyo, kulikuwa na neno la Bwana kwa wote ambao wangechukua muda kulizingatia.

Katika kile kilichoonekana kuwa wakati wa msiba mkubwa, neno la kimya lilizungumza. Baba alitangaza nia yake kimya kimya. Kwa kusema kupitia jina la Simoni, Baba alionyesha kwamba bado alikuwa na mamlaka juu ya mambo ya siku hiyo. Warumi hawakuwa na udhibiti. Akifanya kazi kimyakimya kupitia kile kilichoonekana kuwa mwisho wa kusikitisha, ulikuwa ni mkono wa Baba, ukitimiza kusudi Lake.

Yesu aliposogea polepole kuelekea mahali ambapo angetoa uhai Wake, alimleta Simoni pamoja Naye. Simoni, asiyejulikana, alisema neno la kinabii la Mungu: “Amesikia.” Baba amesikia, na haya ndiyo matokeo. Amemtuma Mwanawe kuutoa uhai wake kama Mwana Kondoo mkamilifu wa Mungu kwa ajili ya ondoleo la dhambi zetu. Kwa kumchagua Simoni kumfuata Mwanawe, Baba alikuwa akitangaza kwamba alikuwa na kusudi katika kile alichokuwa akifanya. Kupitia kazi ya Mwanawe, jibu la vizazi vya maombi lingefichuliwa.

Yakuzingatia:

Jina la Simoni linamaanisha nini? Kwa nini ni muhimu katika

muktadha huu?

Sio watu wengi waliokuwepo siku hiyo wangeelewa ishara kwa jina la Simoni. Kwa nini unadhani Mungu anazungumza kimya kwa njia hii? Je, unafikiri mara nyingi tunakosa kile ambacho Mungu anasema?

Neno la Mungu lililonenwa kupitia jina la Simoni lilidhihirishaje kwamba Yeye bado alikuwa anatawala hali iliyoonekana kwa macho ya wanadamu kuwa kushindwa kabisa?

Maombi:

Mshukuru Bwana kwa kuwa anatawala hata kile kinachoonekana kuwa janga katika maisha yako. Mshukuru kwa faraja anayokuletea katika hitaji lako.

Mshukuru Bwana kwa kuwa anasikia kilio chetu na atajibu kwa njia na wakati wake.

Mwambie Mungu afungue macho na masikio yako kwa faraja anayoleta. Mwambie akupe macho ili uone kile anachofanya katika hali yako.

# Sura ya 5- Kukabidhi Msalaba

Tumeona jinsi Simoni Mkirene alivyomwakilisha Myahudi na mgeni. Katika cheo hiki, alibeba msalaba akifunua kwa wote kwamba sisi tulikuwa wenye hatia ambao tulistahili kufa kwa ajili ya uasi wetu dhidi ya Bwana Yesu, Mwana wa Mungu.

Luka 23:26 inatuambia kwamba Simoni alipokuwa akitembea kwenye barabara hiyo hadi mahali pa kunyongwa, aliubeba msalaba "nyuma ya Yesu." Hebu tusimame kwa muda na tufikirie kile ambacho lazima kilikuwa kikiingia akilini mwa Simoni. Alikuwa amebeba msalaba akielekea Golgotha. Katika hali ya kawaida, hili lingekuwa jambo gumu sana kufanya. Wengi wa wale waliobeba msalaba walikuwa na uzito mkubwa wa kihisia. Msalaba huu ulikuwa ishara ya kifo na mateso yajayo. Ilikuwa mwisho wa maisha kwa mhalifu mwenye hatia. Walipokuwa wakitazama mbele, wale waliohukumiwa walifahamu kikamilifu uhalifu wao na woga wa kile kilichokuwa mbele yao. Wangeinuliwa ili wote wawaone. Wangeteseka sana hadi maisha yao yakafifia. Watu wangewadhihaki na kuwatukana walipokuwa wakining'inia wakifa kwenye msalaba huo wa kikatili. Walipunguzwa kuwa wanyonge na kukata tamaa kwa njia ya umma sana. Msalaba uliundwa ili kuleta usumbufu na aibu ya hali ya juu.

Hebu tumrudie Simoni Mkirene. Ingawa kubeba msalaba lilikuwa jambo zito sana kwake, kulikuwa na kitu tofauti sana katika kesi yake.

Asingefia kwenye msalaba aliobeba. huu ulikuwa kwa ajili ya Yesu. Maumivu na uchungu ungezaliwa na mtu aliyekuwa akimpeleka Golgotha. Simoni alijua kwamba watakapofika Kalvari, atamkabidhi Bwana Yesu msalaba huo.

Simoni Mkirene ni ishara yenye nguvu ya kile kilichotokea kwenye msalaba wa Yesu. Kama mwakilishi wa Wayahudi na wageni, Simoni alibeba msalaba wa Yesu. Ingawa viongozi wa kidunia walikuwa wamemhukumu Yesu kuwa na hatia, Baba pia alifunua hukumu Yake siku hiyo. Alimfanya Simoni kubeba uzito wa msalaba hadi Kalvari. Aliwaonyesha wale waliokuwepo kwamba wao ndio wenye hatia, si Yesu.

Simoni anafanya mengi zaidi ya kufichua hukumu ya Mungu, hata hivyo, anaonyesha pia rehema na huruma ya Mungu katika Bwana Yesu, Mwanawe. Simoni alipofika Golgotha, alimkabidhi Yesu msalaba. Yesu kwa hiari aliweka mwili wake juu ya msalaba huo kwa ajili ya Simoni kama mwakilishi wa Wayahudi na wageni. Kifo cha Yesu kilikuwa kwa niaba yetu. Alilipa adhabu ambayo tulipaswa kulipa.

Sherehe kubwa ilifanyika siku hiyo. Kama mwakilishi wetu, Simoni aliweka boriti ya msalaba chini na kurudi nyuma. Kisha Yesu alilazwa msalabani mahali pa Simoni. Askari walimpigilia misumari kwenye viganja vya mikono na miguu, naye akainuliwa juu ili wote wamuone.

Tunapoangalia hadithi kutoka kwa mtazamo wa Simoni, sio tu kuhusu uamuzi wa viongozi wenye wivu wa kumuua Yesu ili kuhifadhi nafasi zao na njia ya maisha. Inahusu kifo mbadala. Ni kuhusu Yesu

kufa kwa niaba yetu. Ni kuhusu upande usio na hatia kuchukua nafasi ya wenye hatia. Ni kuhusu mwenye hatia kuwekwa huru kutokana na ukali wa hukumu ya Mungu.

Simoni Mkirene alikuwa njia ya Mungu ya kuwasilisha ujumbe wa injili. Imefichwa katika hadithi ya msalaba wa Kristo ni mfano huu wenye nguvu wa Simoni. Hakuwa tu mpita njia, alikuwa chombo cha Mungu kuwasiliana na ulimwengu kile ambacho Yesu alitufanyia. Anatukumbusha kwamba Mungu huwagusa wale wasiopendezwa Naye na kuwashurutisha kumfuata Mwana wake. Yeye ni faraja kwa sisi tulio na wapendwa ambao hawajaokoka. Simoni pia ni ukumbusho kwetu kwamba Mungu ndiye anayesikia kilio chetu. Anatuonyesha kwamba Mungu huchukua mahitaji yetu kwa uzito na atajibu kwa baraka kwa wakati Wake. Ni wito wa kumwamini Mungu anayesikia.

Hatimaye, Simoni anatufundisha kuhusu kifo mbadala cha Kristo. Yesu alikufa badala yetu. Hakuna swali kwamba tulikuwa na hatia mbele za Mungu. Kama Simoni, tulibeba uzito wa msalaba kwenye mabega yetu. Tulikuwa tayari tunaelekea mahali pa kusulubishwa, ambapo tungetesekana hukumu ya Mungu kwa ajili ya dhambi na uasi. Kama Simoni, hata hivyo, tulikabidhi hukumu hiyo kwa Bwana Yesu. Hapo mbele zake, tulisimama, tukiwa na boriti ya msalaba mabegani mwetu, kama wenye dhambi wenye hatia waliohukumiwa na kuhukumiwa kifo. Tunapomkaribia Kristo, hata hivyo, tunasikia wito wa kuweka chini mzigo wa msalaba, kuuweka miguuni pake, na kurudi nyuma. Tunaporudi nyuma, tukijua kabisa hatia yetu, tunamtazama Bwana Yesu akitembea kwenye msalaba huo na

kujilaza juu yake badala yetu. Alichukua uchungu na uchungu wote. Alilipa bei ambayo nilipaswa kulipa. Hukumu yangu imetekelezwa. Adhabu yangu imelipwa. Niko huru kutokana na hatia na aibu niliyobeba. Yesu alichukua yote juu Yake.

Je, unatambua kwamba umepungukiwa na kiwango cha Mungu? Je, unakubali ukweli kwamba umehukumiwa kuwa mwenye dhambi? Je, utauchukua msalaba wako ukikubali hatia hii mbele za Mungu? Je, ukiikubali dhambi yako kikamilifu, utaleta aibu yako kwa Yesu na kuiweka miguuni pake, ukikiri kushindwa kwako na uasi wako kwake? Je, basi utamuachia Yeye hatia hiyo? Je, utakiri leo kwamba Yesu aliyatoa maisha yake kwa ajili yako juu ya msalaba huo? Je, sasa unaweza kutembea kwa ushindi juu ya hukumu yako, ukimsifu na kujitoa kwa Yeye aliyechukua nafasi yako? Mungu ampe kila msomaji neema ya kukubali kazi hii kuu na ya huruma ya Kristo kwa niaba yetu.

Yakuzingatia:

Je, unahisi kwamba Simoni alikuwa chaguo la nasibu la askari au chombo cha Mungu kwa kusudi fulani? Eleza.

Je, Simoni anaonyeshaje ujumbe wa Injili?

Je! ni tofauti gani kati ya jinsi ulimwengu ulivyoona kusulubishwa na jinsi Mungu alivyoona kama ilivyoonyeshwa katika Simoni?

Je, umemjia Kristo na dhambi yako? Je, umetupa hukumu yako kwake?

Maombi:

Mshukuru Bwana Yesu kwa kuchukua adhabu yako. Mwombe akusaidie kuishi sasa kama mtu ambaye umesamehewa na kuwekwa huru kutoka kwenye mzigo wa dhambi.

Mshukuru Bwana kwa kuwa hakuna kinachotokea kwa bahati. Mshukuru kwamba yuko katika kila maisha yako. Hata wapita njia kama Simoni wana kusudi katika moyo wa Mungu.

Ikiwa hujawahi kuelewa kusudi la msalaba wa Yesu, chukua muda sasa kufungua moyo wako kwa kazi Yake kwa niaba yako. Tambua dhambi yako na hitaji la msamaha. Njoo kwa Bwana Yesu na hatia yako na umwombe akusamehe.

# Light To My Path Book Distribution

Light To My Path Book Distribution (LTMP) ni huduma ya uandishi na usambazaji wa vitabu inayowafikia wafanyakazi Wakristo wenye uhitaji huko Asia, Amerika Kusini, na Afrika. Wafanyakazi wengi Wakristo katika nchi zinazoendelea hawana nyenzo zinazohitajika ili kupata mazoezi ya Biblia au kununua vifaa vya kujifunzia Biblia kwa ajili ya huduma zao na kujitia moyo.F. Wayne Mac Leod ni mwanachama wa Action International Ministries na amekuwa akiandika vitabu hivi kwa lengo la kuvisambaza bure au kwa gharama kwa wachungaji wenye uhitaji na wafanyakazi Wakristo kote ulimwenguni.

Vitabu hivi vinatumika katika mahubiri, mafundisho, uinjilisti na kutia moyo waamini wenyeji katika zaidi ya nchi sitini. Vitabu sasa vimetafsiriwa katika lugha kadhaa. Lengo ni kuvifanya vipatikane kwa waumini wengi iwezekanavyo.

Huduma ya LTMP ni huduma yenye msingi wa imani na tunamwamini Bwana kwa nyenzo zinazohitajika ili kusambaza vitabu kwa ajili ya kuwatia moyo na kuwaimarisha waumini duniani kote. Je, ungeomba kwamba Bwana afungue milango kwa ajili ya tafsiri na usambazaji zaidi wa vitabu hivi?

Kwa taarifa Zaidi kuhusuLight To My Path tembelea tovoti yetu ya [www.lighttomypath.ca](http://www.lighttomypath.ca)